Ramadan

# RUWAZA YA KWELI YA MABADILIKO

﴿شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ﴾

Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi.” [Al-Baqarah: ١٨٥]

Mwezi mtukufu wa Ramadhan unatukumbusha kwamba Uislamu ulikuja tu kubadilisha ulimwengu na kutatua matatizo ya wanadamu kulingana na muongozo wa Mwenyezi Mungu (swt) na kwa ruwaza iliyowasilishwa katika Quran na Sunnah. Tunaposhuhudia dhulma, ukandamizaji, na misiba mingi na matatizo yanayoukumba ulimwengu wa Kiislamu na wanadamu kwa jumla, ni wazi kabisa kwamba tunahitaji sana ruwaza sahihi ya mabadiliko iliyo wasilishwa na Uislamu.

Mfumo wa sasa wa dunia ulioharibika, pamoja na nidhamu yake inayoegemea utawala, taasisi na vyombo, unaporomoka mbele ya macho yetu. Dola na mashirika yake yameonekana kutokuwa na uwezo wa kutoa suluhisho thabiti, endelevu na lenye mafanikio kwa matatizo ya mataifa, au kukomesha mauaji ya halaiki, uvamizi na ukandamizaji mkubwa dhidi ya Waislamu na watu wengine. Kwa wakati huu, ni muhimu sana kwamba sisi kama Waislamu tuchukue dori kuu na ya kuongoza katika kuwasilisha mfumo wa haki, imara, wenye mafanikio na sahihi ambao wanadamu wanapaswa kuutazama ili kushughulikia migogoro mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na mengineyo inayoikumba dunia hii.

Mwezi mtukufu wa Ramadhan unapaswa kuwa fursa kwetu kuelewa na kutafakari ruwaza ya kweli ya mabadiliko ya wanadamu kama ilivyowasilishwa katika Quran na Sunna, jinsi ya kuifikia, na dori yetu kama Waislamu katika kufikia lengo hili.

Ramadhan hii, Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir kitazungumzia maudhui hii, ikiwa ni pamoja na sifa na mabadiliko yanayohitajika kwetu kama Waislamu, kama Umma wa Kiislamu, katika vyama vyetu vya kisiasa, majeshi yetu, na katika ngazi ya dola, ili kufikia ruwaza hii ya kweli ya mabadiliko, pamoja na vikwazo vinavyozuia kuifikia na jinsi ya kuvishinda. Tunato wito kwenu kufuatilia na kuunga mkono mada yetu ya Ramadhan kupitia kusambaza mabango, makala na majadiliano katika kurasa zetu ambayo yatachapishwa katika kipindi kizima cha mwezi huu mtukufu.

﴿وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَانًا لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَىٰ لِلْمُسْلِمِينَ﴾

“Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu,na rehema, na bishara kwa Waislamu.” [An-Nahl: ٨٩]

RAMADAN
EMBRACING THE
TRUE VISION FOR CHANGE

#TrueVision4Change